Muhtasari wa Sera TZ.03/2011K

# Matokeo yakipuuzwa, ukaguzi wa nini?

## Tunachojifunza kutoka katika miaka mitano ya ukaguzi wa Serikali za Mitaa








## 1. Utangulizi

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2005/6-2009/10) ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekagua hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuwasilisha matokeo ya ukaguzi huo Bungeni pasipo kuchelewa. Kuna sababu kadhaa za kufanya ukaguzi. Mojawapo ni kuhakikisha kwamba taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaakisi (vema) yale yanayofanyika, na iwapo kanuni zilizowekwa zinazingatiwa. Makosa au ukiukwaji wa taratibu unapogundulika, inatarajiwa kwamba dosari hizo zitarekebishwa. Hivyo, dhima nyingine muhimu ya ukaguzi wa hesabu ni kuhakikisha kuwa ubora wa usimamizi wa fedha za umma unaimarika siku hadi siku. Lakini, je, hivi ndivyo hali halisi ilivyo?

Muhtasari huu unatumia ripoti za ukaguzi wa hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kutathmini mabadiliko katika ubora wa usimamizi wa fedha katika Mamlaka hizo katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Tathmini inaonesha kwamba viwango vya ubora wa hati za ukaguzi havikupanda na kwamba hata baada ya miaka mitano ya ukaguzi, usimamizi wa fedha katika Mamlaka nyingi za Serikali za Mitaa bado ni dhaifu. Kwa kiasi kikubwa mapendekezo kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali yanapuuzwa, na hata hoja za ukaguzi hazifanyiwi kazi jambo linaloibua maswali kuhusu umuhimu wa kufanya ukaguzi huo wa hesabu. Kuna sababu gani za kufanya ukaguzi iwapo matokeo yake hayatumiwi katika kurekebisha utendaji mbovu katika usimamizi wa fedha?

Bila shaka njia bora inayofaa kufuatwa si kuacha kuendesha ukaguzi wa fedha bali kuhakikisha kwamba changamoto za kiukaguzi zinashughulikiwa ipasavyo. Muhtasari huu unapendekeza kwamba Tanzania iweke vichocheo vitakavyohakikisha kwamba mapendekezo yanayotokana na ukaguzi yanafanyiwa kazi. Mamlaka inayoteua timu za menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wabunge, Kamati za Uwajibikaji za Bunge, na Wajumbe wa Halmashauri wana wajibu mkubwa katika kuhakikisha kwamba jambo hili linafanikiwa.

Muhtasari huu umeandaliwa na Rose Aiko wa Uwazi iliyoko Twaweza-Hivos Tanzania.

Uwazi, S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301. Nukushi: +255 22 266 4308.
Baruapepe: info@uwazi.org. Tovuti: www.uwazi.org
Umetolewa Mei, 2011

## 2. Hati za ukaguzi

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anapokamilisha ukaguzi wa hesabu za halmashauri inayohusika hutoa hati (maoni) ya kitaalamu. Hati hizi hutoa viashiria iwapo taarifa za hesabu za halmashauri husika zinawasilisha kwa usahihi matokeo ya shughuli zake, mtiririko wa fedha na picha kamili ya mwenendo wa mapato na matumizi ya fedha kwa ujumla. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anaweza kutoa hati za aina tatu: hati inayoridhisha (ambayo pia hujulikana kama hati safi ya ukaguzi); hati yenye mashaka (au hati isiyo safi); na hati isiyoridhisha. Hati hii ya mwisho huashiria uwepo wa kasoro kubwa katika taarifa za kifedha za halmashauri.

Hati zinazoridhisha ni za aina mbili, hati safi bila masuala ya msisitizo na hati safi yenye masuala ya msisitizo kwenye maeneo fulani. Hati safi ya ukaguzi isiyo na masuala ya msisitizo ndiyo nzuri zaidi. Wakati mwingine Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali hukataa kutoa hati ya kitaalamu na hapo hutoa hati mbaya. Hii ndiyo hati iliyo mbaya zaidi. Hati hii hutolewa wakati ambapo taarifa za hesabu zimetayarishwa vibaya sana kiasi kwamba humwia vigumu hata Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kutathmini ukweli na kuaminika kwa hesabu zilizokaguliwa.

- **Hati safi ya ukaguzi isiyo na masuala ya msisitizo** ina maana kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ameridhika kwamba taarifa za mahesabu ya halmashauri husika zinawasilisha hali ya kifedha ya halmashauri kwa kiwango cha usahihi kinachoridhisha.[1]
- **Hati safi ya ukaguzi yenye msisitizo kwenye maeneo fulani** inaonesha kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali hakuridhishwa kikamilifu na taarifa za hesabu zilizowasilishwa kwake. Msisitizo huo unafanywa ili kumjulisha afisa masuuli, yaani, mkurugenzi wa halmashauri, kuhusu masuala anayotakiwa kuyafanyia kazi bila kuchelewa.
- **Hati isiyo safi (hati yenye mashaka)** inatolewa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anapohitimisha kwamba japo taarifa za fedha zinazingatia utaratibu au kanuni za uandaaji wa taarifa za kifedha bado kuna masuala yanayofanya ripoti hiyo ya hesabu kutiliwa mashaka. Kutokana na mashaka hayo hati safi haiwezi kutolewa.
- Iwapo halmashauri inapata **hati isiyoridhisha**, maana yake ni kwamba taarifa za hesabu za halmashauri zimeonekana hazikutayarishwa kulingana na misingi inayokubalika ya utayarishaji wa taarifa za fedha au zina kasoro nyingi na hivyo zinapotosha kabisa.
- **Hati mbaya** maana yake ni kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anakataa kutoa hati (maoni ya kitaalamu) kwa sababu hakuweza kupata ushahidi wa kutosha na unaoridhisha katika taarifa za fedha kumwezesha kutoa maoni ya kitaalamu kuhusu kuaminika kwa hali ya fedha ya halmashauri.

## 3. Tunajifunza nini kutokana na miaka mitano ya ukaguzi wa Serikali za Mitaa


### Somo la 1: Hali ya usimamizi wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa inaendelea kuzorota

Idadi ya hati safi (hati zinazoridhisha) zinazotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali inabadilika kila mwaka. Ikilinganishwa na zile zilizotolewa mwaka 2005/06 hakuna ushahidi unaoonesha kuongezeka kwa jumla kwa viwango vya ubora katika miaka mitano iliyopita. Kwa kweli, baada ya viwango kukua kati ya mwaka 2005/06 na mwaka 2006/07 ubora wa usimamizi wa fedha unaonekana kudidimia – hasa tunapoupima dhidi ya kigezo cha maoni ya kitaalamu ya mkaguzi (Kielelezo cha 1).

[1] Kutokuwepo kwa msisitizo kuhusu maeneo yanayohitaji kufanyiwa kazi hakuna maana kwamba halmashauri haina kabisa maeneo kama hayo. Kwa sabanu hiyo, kwa kawaida Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali hutoa waraka ambatanishi kwa menejimenti za halmashauri husika unaoeleza mambo gani yanahitaji kufanyiwa marekebisho.

Ishara dhahiri ya kudidimia kwa usimamizi wa fedha ni kwamba katika mwaka 2009/10 idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopata hati zisizoridhisha (65) ni sawa na zile zilizopata hati ya kuridhisha. Vilevile, idadi ya hati mbaya iliongezeka (kutoka 0 katika mwaka 2006/07 hadi kufikia 4 katika mwaka 2009/10). Wakati ambapo katika mwaka 2005/06 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali alitoa hati tatu zinazoridhisha bila masuala ya msisitizo, aina hii ya hati haijatolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa tangu wakati huo. Kwa maneno mengine ni kwamba katika miaka minne iliyopita Mamlaka za Serikali za Mitaa zote zilikuwa na matatizo makubwa katika usimamizi wao wa fedha ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali aliona ni muhimu kuyabainisha kwa uongozi wa halmashauri na kwa umma.

**Kielelezo cha 1: Mwelekeo wa hati za ukaguzi zilizopokelewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa: mwaka 2005/06 - 2009/10**




**Chanzo cha data:** Ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa

## Somo la 2: Idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye kasoro katika usimamizi wa fedha imeongezeka

Kila Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anapokagua Mamlaka za Serikali za Mitaa, anapendekeza hatua za marekebisho ya kufanywa ili kuhakikisha mapungufu/ kasoro zinazofanana na zile alizobainisha hazirudiwi tena. Maafisa masuuli, ambao katika halmashauri ni Wakurugenzi wa Halmashauri, wanatarajiwa kutekeleza mapendekezo haya. Hali halisi inaonesha mapendekezo hayo hayafanyiwi kazi vilivyo kwani kasoro zilezile bado zinaendelea kuonekana na huathiri Mamlaka za Serikali za Mitaa nyingi zaidi kila mwaka. Inadhihirisha kwamba mapendekezo yanayotolewa hayachukuliwi kwa uzito unaostahili.

Orodha ya kasoro zinazojitokeza mara kwa mara na kiwango cha kujirudia kwake kati ya mwaka 2005/06 na 2009/10 zimeorodheshwa hapa chini. Kiasi cha fedha kinachohusishwa katika hoja zilizoibuliwa na kaguzi zilizotangulia ambazo hazikutolewa maelezo, kushindwa kutumia fedha za ruzuku za maendeleo kwa muda uliopangwa, na kuingia katika mikataba iliyo nje ya uwezo wa kifedha wa halmashauri ni miongoni mwa mambo yaliyohusisha zaidi ya halmashauri 100 katika mwaka 2009/10. Idadi hii ni mara mbili ya ile ya mwaka 2005/06.

**Jedwali la 1: Taratibu zilizokiukwa na zinazojitokeza mara nyingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na idadi ya halmahauri zinazohusika**

| Taratibu zilizokiukwa | Idadi ya Halmashauri zilizohusika | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2005/06 | 2006/07 | 2007/08 | 2008/09 | 2009/10 |
| Kiasi cha hoja za mkaguzi kutoka kaguzi zilizotangulia ambazo hazikufanyiwa kazi | 65 | 52 | 112 | 126 | 129 |
| Wadaiwa wasiolipa | 45 | 76 | 115 | 113 | 109 |
| Wadai wasiolipwa (madeni) | 47 | 68 | 101 | 113 | 113 |
| Karadha na masurufu ambayo hayakurejeshwa/ yaliyolipwa yenye mashaka | 16 | 17 | 17 | n.a | n.a |
| Maduhuli ambayo hayajarejeshwa na Mawakala wa kukusanya mapato | 14 | 12 | 22 | 43 | 43 |
| Vitabu vya maduhuli havikuonekana wakati wa ukaguzi | 35 | 8 | 43 | 50 | 48 |
| Malipo yenye nyaraka pungufu | 46 | 32 | 69 | 63 | 71 |
| Hati za malipo hazikuonekana wakati wa ukaguzi | 27 | 12 | 45 | 33 | 34 |
| Ruzuku za maendeleo ambazo hazikutumiwa(bakaa) | 5 | 14 | 111 | 118 | 127 |
| Mishahara ambayo haikulipwa na fedha hazikurejeshwa hazina | 26 | 28 | 71 | 58 | 55 |
| Mishahara iliyolipwa kwa wastaafu, watoro, na watumishi walioachishwa kazi | n.a | n.a | 19 | 40 | 38 |


n.a: Suala ambalo halikuongelewa waziwazi katika mwaka huo

**Chanzo cha data:** Ripoti za Mkaguzi Mkuu kuhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa

## Somo la 3: Mifumo ya udhibiti wa kifedha ndani ya Halmashauri ni dhaifu

Ukaguzi wa hivi karibuni umetathmini hali ya mifumo ya udhibiti wa kifedha ya ndani katika halmashauri zote nchini. Ukaguzi huo uligundua hali ya kusikitisha. Mwaka 2009/10, halmashauri 115 kati ya 134 zilikutwa zina mifumo ya udhibiti wa fedha isiyokidhi mahitaji. Katika asilimia 64 ya halmashauri (Halmashauri 86) mazingira ya udhibiti wa ndani yalikuwa duni. Na licha ya kuwepo teknolojia na Serikali kuhimiza utawala unaoendeshwa kielektroni (e-Governance), zaidi ya theluthi ya halmashauri zilikuwa zikiandaa hesabu zake kwa mkono (zina mifumo ya fedha isiyotumia kompyuta) hali inayoweza kusababisha makosa mengi kufanyika, na makosa hayo kulundikana kutokana na kutobainika kirahisi.

**Kielelezo cha 2: Kasoro katika mfumo wa udhibiti wa ndani katika halmashauri: mwaka 2009/10**




**Chanzo cha data:** Ripoti za Mkaguzi Mkuu kuhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2009/10


## Somo la 4: Serikali za Mitaa zinashindwa kujibu hoja za mkaguzi kikamilifu

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anapohoji yaliyomo katika taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa au kuhusu hali ya mfumo wa udhibiti wa ndani, anatoa pia mapendekezo. Menejimenti za Halmashauri zinatarajiwa kuzifanyia kazi hoja hizo kabla ya ukaguzi unaofuata na maafisa masuuli wanatarajiwa kumjulisha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali namna hoja hizo za ukaguzi zitakavyofanyiwa kazi.

Ushahidi unaonesha kwamba hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali huwa hazifanyiwi kazi. Vilevile idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye hoja za ukaguzi zisizojibiwa kikamilifu imeongezeka. Mwaka 2005/06 halmashauri 65 tu ndizo zilikuwa na hoja za ukaguzi ambazo hazikuwa zimefanyiwa kazi na kupatiwa majibu ya kuridhisha. Mwaka 2009/10 karibu Mamlaka zote za Serikali za Mitaa zilikuwa na hoja zisizojibiwa kikamilifu: ni Mamlaka 5 tu (Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Halmashauri ya Mji wa Njombe, Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, Halmashauri ya Wilaya ya Chato na Halmashauri ya Manispaa ya Songea) ndizo hazikuwa na malimbikizo ya fedha katika hoja za ukaguzi ambazo hazikufanyiwa kazi kutoka kaguzi zilizotangulia.

Kwa kuwa mapendekezo ya mkaguzi hayafanyiwi kazi, kiasi cha fedha kinachohusishwa katika hoja za mkaguzi ambazo hazikutekelezwa kimeendelea kuongezeka (Kielelezo cha 3). Kiasi cha fedha katika hoja za mkaguzi ambazo hazikufanyiwa kazi kilikuwa Shilingi bilioni 9 mwaka 2005/06; mwaka 2009/10, kiasi hicho kimeongezeka hadi kufikia Shilingi bilioni 122, karibu mara kumi na nne zaidi ya kiasi cha mwaka 2005/06.

**Kielelezo cha 3: Jinsi Mamlaka za Serikali za Mitaa zinavyochangia kuongezeka kwa hoja za mkaguzi ambazo hazikufanyiwa kazi**




**Chanzo cha data:** Ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa

## Somo la 5: Kuna halmashauri chache zenye mwelekeo unaoonesha matumaini

Kama inavyooneshwa katika Kielelezo cha 1 na 3, idadi ya halmashauri zenye hati ya mkaguzi inayoridhisha imeendelea kushuka polepole kutoka 100 katika mwaka 2006/07 hadi 65 mwaka 2009/10, ambapo kiasi cha fedha katika hoja ambazo hazikufanyiwa kazi imeendelea kukua kwa kiasi kikubwa.

Kwa kutumia mpango wa alama kutoka 0-3 ambapo 0 inawakilisha 'hati mbaya' na 3 inawakilisha 'hati safi ya ukaguzi isiyo na masuala ya msisitizo, tunaweza kuonesha maendeleo katika ubora wa hati za ukaguzi ulivyotokea. Pia tunaweza kuonesha halmashauri zilizofanya vizuri na zilizo-fanya vibaya katika kipindi cha miaka mitano kwa mujibu wa alama zinazoambatana na hati zao


za ukaguzi. Uchambuzi unaonesha kwamba alama ya jumla kwa halmashauri zote katika mwaka 2009/10 ni 1.4, kama ilivyokuwa katika mwaka 2005/06[2] (tazama Kiambatisho ili kupata taarifa kamili kuhusu nafasi kwa kila halmashauri). Wastani wa jumla katika kipindi cha miaka mitano ni 1.5, kukiwa na halmashauri chache sana (14 kati ya 133) zilizopata alama 2. Halmashauri hizi ni pamoja na halmashauri 10 tu zilizopata hati safi katika kipindi chote cha miaka mitano iliyopita (Halmashauri za wilaya ya Karatu, Mufindi, Kilolo, Kiteto, Mbulu, Kwimba, Tunduru, Manyoni, na Halmashauri za Manispaa za Shinyanga na Morogoro); halmashauri tatu changa zilizoanzishwa mwaka 2007 (halmshauri za Arusha, Misenyi, na Siha) ambazo zilifanikiwa kupata hati safi ya ukaguzi mfululizo katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita; na Halmashauri ya wilaya ya Hai, moja kati ya halmashauri chache zilizofanikiwa kupata hati safi ya ukaguzi bila msisitizo mwaka 2005/06.

Kwa kuzingatia namna halmashauri zinavyotekeleza hoja za mkaguzi, tunaona kwamba katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, Halmashauri ya Mji wa Njombe ndiyo pekee ambayo haikuwa na masuala yaliyohitaji kufanyiwa kazi katika mwaka wowote. Kuwepo kwa Halmashauri ya Njombe kama mtendaji bora zaidi katika kufanyia kazi hoja za mkaguzi kunadhihirisha kwamba halmashauri nyingine hazina sababu za msingi zinazofanya zishindwe kutekeleza kikamilifu hoja za ukaguzi.

## Somo la 6: Usimamizi katika kukusanya maduhuli (mapato) ni dhaifu

Mamlaka za Serikali za Mitaa zina wajibu wa kukusanya mapato katika sehemu zao ili kuongezea katika fedha zinazopokea kutoka Serikali kuu na zimeruhusiwa kutumia mawakala kukusanya mapato hayo. Wakati mawakala wanapotumiwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa zina jukumu la kuwasimamia ili kuhakikisha wanafanya marejesho timilifu ya maduhuli. Ukaguzi umeonesha kwamba mara nyingi Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashindwa kufanya hivyo. Mathalani, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashindwa kuhakikisha kwamba mawakala wanaipa halmashauri fedha zote walizozikusanya. Katika mwaka 2009/10 kiasi cha mapato ambacho hakikuwasilishwa kwa halmashauri kilikuwa Shilingi bilioni 2.76, ambacho ni takriban mara kumi na mbili zaidi ya kile cha mwaka 2005/06 (Kielelezo cha 4).

**Kielelezo cha 4: Mapato yasiyowasilishwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na mawakala wakusanyaji**





**Chanzo cha data:** Ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa

[2] Halmashauri 14 kati ya 134 ni changa; zilianzishwa baada ya mwaka 2006. Kwa halmashauri hizi, alama ya wastani kwa kipindi cha miaka mitatu inadhaniwa kuwa ndiyo nzuri zaidi ambayo zingeweza kupata kama zingekaguliwa kwa miaka mitano, yaani ikiwemo miaka ya 2005/06 na 2006/7. Mamlaka ya Mji wa Kondoa haikujumishwa kwenye alama ya jumla.

Vilevile, vitabu vingi sana vya kukusanya mapato vinapotea kila mwaka (Kielelezo cha 5). Ni wazi kwamba mara chache kitabu kinaweza kupotea lakini hali hii ikitokea sheria inawataka maafisa masuuli watoe taarifa mara moja kuhusu upotevu huo kwa vyombo vinavyohusika. Lakini kinyume na jinsi sheria inavyoagiza, kuna vitabu vingi sana vya risiti vinavyotumiwa kukusanya maduhuli vinavyopotea bila kutolewa taarifa. Ni vigumu kujua iwapo vitabu hivyo ambavyo havikupatikana ili vikaguliwe vilitumika kukusanya fedha, na iwapo jambo hili lilifanyika katika njia halali (yaani, iwapo fedha zilizokusanywa kwa kutumia vitabu hivyo ziliwasilishwa katika halmashauri au la).

**Kielelezo 5: Vitabu vya kukusanyia maduhuli vilivyopotea**





**Chanzo cha data:** Ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa

## Somo la 7: Fedha nyingi zinazopelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatumiwa kwa namna inayoleta mashaka

Malipo yanayotiliwa mashaka ni kama vile malipo yaliyofanyika bila hati za malipo kuambatishwa malipo yenye nyaraka pungufu (ambazo hazijitoshelezi kimaelezo), bidhaa na huduma ambazo zimelipiwa lakini hazikupokelewa, mishahara iliyolipwa kwa wafanyakazi hewa (waliostaafu, watoro na/au walioachishwa kazi) na masurufu na karadha ambazo au zinalipwa kinyume na taratibu za kisheria au hayatolewi maelezo kikamilifu ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha.

Katika mwaka 2006/07 matumizi yenye kutiliwa mashaka yalipungua kwa kiasi kikubwa, hali inayoonesha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweza kufanya matumizi kwa kufuata taratibu na kanuni za kifedha zilizowekwa ipasavyo. Hata hivyo tangu wakati huo hali imebadilika, na katika mwaka 2009/10 matumizi yenye kutiliwa mashaka yamefikia Shilingi bilioni 9.2. Kiasi kilicholimbikizwa katika kipindi cha miaka mitano kinafika Shilingi bilioni 33.4. Kiasi hiki ni zaidi ya kile kinachohitajika kujenga vyoo vya kutosheleza mahitaji katika shule za sekondari za Serikali; kujenga miundombinu na kuwezesha upatikanaji wa vifaa kwa ajili ya michezo nje ya darasani na kuwafadhili kwa kuwalipia gharama za masomo wanafunzi takriban 80,000 wanaotoka katika familia zenye uwezo mdogo kwa miaka mitano.

**Kielelezo cha 6: Fedha zaidi zinatumiwa na Halmashauri katika malipo yenye mashaka**





| | 2005/6 | 2006/7 | 2007/8 | 2008/9 | 2009/10 |
|---|---|---|---|---|---|
| Masurufu ambayo hayakurejeshwa | .807 | .587 | .214 | - | - |
| Mishahara kwa wafanyakazi hewa | - | - | .178 | .793 | .583 |
| Malipo kwa huduma/bidhaa ambazo hazikupokelewa | .480 | 1.006 | .697 | 1.835 | .240 |
| Malipo yasiyokuwa na hati za malipo | 1.934 | .081 | 1.370 | 2.526 | 2.830 |
| Nyaraka za malipo zina mapungufu | 2.403 | .895 | 3.590 | 5.313 | 5.515 |

"-" Jambo hili halitajwi waziwazi katika ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali katika mwaka huo
**Chanzo cha data:** Ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa

## Somo la 8: Fedha nyingi zaidi za miradi ya maendeleo hazitumiwi kwa wakati

Halmashauri zinaposhindwa kutumia fedha zilizotengwa kwa miradi ya maendeleo kwa wakati uliopangwa mambo mawili hujitokeza. Kwanza, huduma na manufaa yaliyokusudiwa kwa jamii yanacheleweshwa. Na pili, kwa sababu gharama zinaendelea kupanda na kwa vile mfumuko wa bei unashusha thamani ya fedha iliyotengwa katika bajeti, ni huduma chache tu ndizo zinazoweza kupatikana ikilinganishwa na zile zilizopangwa awali. Licha ya matatizo haya kujulikana wazi, bado halmashauri nyingi hazitumii ruzuku za maendeleo kikamilifu na kwa wakati uliopangwa ili kuwafikishia wananchi huduma muhimu. Mwaka 2009/10 peke yake, inakisiwa kuwa asilimia 35 ya ruzuku za maendeleo zilizogawiwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikutumiwa zote kama ilivyokusudiwa. Katika fedha halisi, kiasi cha fedha za maendeleo ambazo hazikutumika mwaka 2009/10 ni karibu mara 65 ya kiasi cha fedha ambazo hazikutumiwa katika mwaka 2005/06.

**Kielelezo 7: Fedha nyingi za miradi ya maendeleo hazitumiwi ndani ya kipindi kilichopangwa**




**Chanzo cha data:** Ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa

## 4. Hitimisho

Muhtasari huu umeonesha kwamba licha ya kufanyika ukaguzi kwa miaka mitano mfululizo, udhibiti wa kifedha ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa bado ni dhaifu na mapendekezo ya kutatua kasoro zilizobainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali yanapuuzwa. Mwelekeo wa ubora wa hati za ukaguzi katika kipindi cha miaka michache iliyopita umeonesha kuzorota na usimamizi wa fedha unaonekana kuwa mbaya zaidi. Hata hivyo, kuwapo kwa halmashauri zinazofanya vizuri, japo ni chache, kunadhihiridha kwamba kukiwa na kiwango cha kuridhisha cha utashi wa kuwajibika halmashauri nyingine nazo zitaongeza ufanisi katika utendaji wao.

Hizi ni sababu zinazoshawishi kwamba kuna haja ya mapendekezo ya ukaguzi kupokelewa kwa uzito unaostahili na kutekelezwa. Na kama data za mwaka 2006/07 zinavyoonesha, mapungufu si lazima yawe ya kudumu. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali mwenyewe mara nyingi amependekeza hatua kadhaa za kuzingatia ili kuziondoa kasoro zilizopo. Baadhi ya hatua hizo tunazirudia hapa:

- Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*Local Authorities Accounts Committee*) inahitaji kutekeleza majukumu yake kwa makini zaidi kwa kuwawajibisha maafisa masuuli wanaoshindwa kusimamia rasilimali za umma ipasavyo. Kamati inaweza kuanzisha na kuratibu mikutano ya wazi (public hearings) ambapo wananchi watashiriki na kuwataka maafisa masuuli kutoa maelezo kuhusu matatizo ya usimamizi wa fedha katika Halmashauri zao.
- Halmashauri ziwe wazi zaidi kuhusu rasilimali zinazokusanya na /au kupokea na kuonesha fedha hizo zinakusudiwa kutumika kwa kazi gani. Ni katika mazingira ya uwazi ndiyo wananchi wanaweza kuimarisha uwajibikaji kwa kuudai katika utoaji wa huduma kwa umma.
- Mamlaka inayoteua maafisa masuuli inahitaji kutekeleza kanuni za uwajibikaji katika ajira kama ilivyopendekezwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu mameneja wanaoshindwa kulinda rasilimali za umma.
- Mamlaka inayoteua ifikirie kuanzisha mfumo wa ajira utakaoilazimisha timu ya menejimenti katika sekta ya umma kuwajibika zaidi. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali amependekeza kuajiri mameneja kwa kanuni za mikataba inayoweza kuongezwa iwapo tu mwajiriwa anaonesha ufanisi katika utendaji kazi.
- Wabunge na Madiwani wafanye kazi ya ziada kwa kuhoji katika mikutano ya halmashauri iwapo wakurugenzi wa halmashauri wanasimamia rasilimali za umma kwa namna inayonufaisha jamii.

Unaweza kujifunza zaidi kuhusu hali ya ukaguzi katika halmashauri mbalimbali kwa kusoma ripoti kamili ya ukaguzi kutoka tovuti ya Ofisi ya Ukaguzi www.nao.go.tz. Kwa uchambuzi zaidi kuhusu ukaguzi na rasilimali za umma tembelea www.uwazi.org

**Kiambatisho: Nafasi za Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokana na ubora wa hati ya ukaguzi iliyopokelewa katika kipindi cha miaka mitano**

| NAFASI | HALMASHAURI | MKOA | 2005/6 | 2006/7 | 2007/8 | 2008/9 | 2009/10 | ALAMA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mufindi DC | **IRINGA** | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2.0 |
| 2 | Karatu DC | **ARUSHA** | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2.0 |
| 3 | Kilolo DC | **IRINGA** | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2.0 |
| 4 | Kiteto DC | **MANYARA** | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2.0 |
| 5 | Mbulu DC | **MANYARA** | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2.0 |
| 6 | Morogoro MC | **MOROGORO** | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2.0 |
| 7 | Kwimba DC | **MWANZA** | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2.0 |
| 8 | Tunduru Dc | **SONGEA** | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2.0 |
| 9 | Shinyanga MC | **SHINYANGA** | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2.0 |
| 10 | Manyoni DC | **SINGIDA** | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2.0 |
| 11 | Arusha DC | **ARUSHA** | N/A | N/A | 2 | 2 | 2 | 2.0 |
| 12 | Misenyi DC | **KAGERA** | N/A | N/A | 2 | 2 | 2 | 2.0 |
| 13 | Siha DC | **KILIMANJARO** | N/A | N/A | 2 | 2 | 2 | 2.0 |
| 14 | Hai DC | **KILIMANJARO** | **3** | 2 | 1 | 2 | 2 | 2.0 |
| 15 | Kisarawe DC | **COAST** | 1 | 2 | 2 | 2 | 2 | 1.8 |
| 16 | Mafia DC | **COAST** | 2 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1.8 |
| 17 | Biharamulo DC | **KAGERA** | 1 | 2 | 2 | 2 | 2 | 1.8 |
| 18 | Bukoba DC | **KAGERA** | 2 | 2 | 1 | 2 | 2 | 1.8 |
| 19 | Muleba DC | **KAGERA** | 2 | 2 | 1 | 2 | 2 | 1.8 |
| 20 | Kasulu DC | **KIGOMA** | 2 | 2 | 1 | 2 | 2 | 1.8 |
| 21 | Kibondo DC | **KIGOMA** | 2 | 2 | 2 | 1 | 2 | 1.8 |
| 22 | Same DC | **KILIMANJARO** | 2 | 2 | 2 | 1 | 2 | 1.8 |
| 23 | Nachingwea DC | **LINDI** | 2 | 1 | 2 | 2 | 2 | 1.8 |
| 24 | Hanang' DC | **MANYARA** | 2 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1.8 |
| 25 | Serengeti DC | **MARA** | 1 | 2 | 2 | 2 | 2 | 1.8 |
| 26 | Chunya DC | **MBEYA** | 2 | 1 | 2 | 2 | 2 | 1.8 |
| 27 | Kyela DC | **MBEYA** | 1 | 2 | 2 | 2 | 2 | 1.8 |
| 28 | Ulanga DC | **MOROGORO** | 2 | 2 | 2 | 1 | 2 | 1.8 |
| 29 | Newala DC | **MTWARA** | 2 | 2 | 2 | 1 | 2 | 1.8 |
| 30 | Sengerema DC | **MWANZA** | 2 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1.8 |
| 31 | Nkasi DC | **RUKWA** | 2 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1.8 |
| 32 | Sumbawanga DC | **RUKWA** | 2 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1.8 |
| 33 | Songea DC | **SONGEA** | 2 | 2 | 2 | 1 | 2 | 1.8 |
| 34 | Bariadi DC | **SHINYANGA** | 2 | 2 | 1 | 2 | 2 | 1.8 |
| 35 | Meatu DC | **SHINYANGA** | 2 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1.8 |
| 36 | Iramba DC | **SINGIDA** | 2 | 2 | 1 | 2 | 2 | 1.8 |
| 37 | Muheza DC | **TANGA** | 2 | 2 | 1 | 2 | 2 | 1.8 |
| 38 | Tabora MC | **TABORA** | 1 | 2 | 2 | 2 | 2 | 1.8 |
| 39 | Mpanda TC | **RUKWA** | N/A | N/A | 2 | 2 | 1 | 1.7 |
| 40 | Njombe TC | **IRINGA** | N/A | N/A | 2 | 2 | 1 | 1.7 |
| 41 | Kibaha TC | **COAST** | 2 | 2 | 2 | 1 | 1 | 1.6 |
| 42 | Rufiji/Utete DC | **COAST** | 1 | 2 | 1 | 2 | 2 | 1.6 |
| 43 | Kinondoni MC | **DSM** | 1 | 2 | 2 | 1 | 2 | 1.6 |
| 44 | Kondoa DC | **DODOMA** | 1 | 2 | 2 | 1 | 2 | 1.6 |
| 45 | Kongwa DC | **DODOMA** | 1 | 2 | 2 | 1 | 2 | 1.6 |
| 46 | Mpwapwa DC | **DODOMA** | 1 | 2 | 2 | 1 | 2 | 1.6 |
| 47 | Bukoba MC | **KAGERA** | 1 | 2 | 1 | 2 | 2 | 1.6 |
| 48 | Karagwe DC | **KAGERA** | 1 | 2 | 2 | 1 | 2 | 1.6 |
| 49 | Ngara DC | **KAGERA** | 2 | 2 | 1 | 1 | 2 | 1.6 |
| 50 | Lindi DC | **LINDI** | 2 | 1 | 1 | 2 | 2 | 1.6 |

| NAFASI | HALMASHAURI | MKOA | 2005/6 | 2006/7 | 2007/8 | 2008/9 | 2009/10 | ALAMA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 51 | Lindi TC | **LINDI** | 1 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1.6 |
| 52 | Babati TC | **MANYARA** | 2 | 2 | 1 | 2 | 1 | 1.6 |
| 53 | Musoma DC | **MARA** | 1 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1.6 |
| 54 | Bunda DC | **MARA** | 1 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1.6 |
| 55 | Musoma MC | **MARA** | 1 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1.6 |
| 56 | Tarime DC | **MARA** | 1 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1.6 |
| 57 | Mbozi DC | **MBEYA** | 1 | 1 | 2 | 2 | 2 | 1.6 |
| 58 | Rungwe DC | **MBEYA** | 2 | 2 | 1 | 1 | 2 | 1.6 |
| 59 | Kilombero DC | **MOROGORO** | 2 | 2 | 1 | 1 | 2 | 1.6 |
| 60 | Masasi DC | **MTWARA** | 1 | 2 | 1 | 2 | 2 | 1.6 |
| 61 | Mtwara DC | **MTWARA** | 1 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1.6 |
| 62 | Tandahimba DC | **MTWARA** | 2 | 1 | 1 | 2 | 2 | 1.6 |
| 63 | Geita DC | **MWANZA** | 1 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1.6 |
| 64 | Misungwi DC | **MWANZA** | 1 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1.6 |
| 65 | Mpanda DC | **RUKWA** | 1 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1.6 |
| 66 | Mbinga DC | **SONGEA** | 2 | 2 | 2 | 1 | 1 | 1.6 |
| 67 | Songea MC | **SONGEA** | 2 | 2 | 1 | 2 | 1 | 1.6 |
| 68 | Bukombe DC | **SHINYANGA** | 1 | 2 | 1 | 2 | 2 | 1.6 |
| 69 | Shinyanga DC | **SHINYANGA** | 2 | 1 | 1 | 2 | 2 | 1.6 |
| 70 | Maswa DC | **SHINYANGA** | 1 | 1 | 2 | 2 | 2 | 1.6 |
| 71 | Singida DC | **SINGIDA** | 1 | 2 | 2 | 2 | 1 | 1.6 |
| 72 | Handeni DC | **TANGA** | 2 | 2 | 2 | 1 | 1 | 1.6 |
| 73 | Pangani DC | **TANGA** | 2 | 2 | 2 | 1 | 1 | 1.6 |
| 74 | Tanga CC | **TANGA** | 2 | 2 | 2 | 1 | 1 | 1.6 |
| 75 | Kilindi DC | **TANGA** | 3 | 1 | 1 | 2 | 1 | 1.6 |
| 76 | Tabora DC | **TABORA** | 1 | 2 | 1 | 2 | 2 | 1.6 |
| 77 | Urambo DC | **TABORA** | 1 | 1 | 2 | 2 | 2 | 1.6 |
| 78 | Bagamoyo DC | **COAST** | 1 | 2 | 2 | 1 | 1 | 1.4 |
| 79 | Kibaha DC | **COAST** | 1 | 2 | 1 | 1 | 2 | 1.4 |
| 80 | Dar es Salaam CC | **DSM** | 1 | 2 | 2 | 1 | 1 | 1.4 |
| 81 | Ilala MC | **DSM** | 2 | 1 | 1 | 1 | 2 | 1.4 |
| 82 | Temeke MC | **DSM** | 1 | 2 | 1 | 2 | 1 | 1.4 |
| 83 | Dodoma MC | **DODOMA** | 1 | 2 | 1 | 2 | 1 | 1.4 |
| 84 | Iringa DC | **IRINGA** | 1 | 2 | 1 | 1 | 2 | 1.4 |
| 85 | Iringa MC | **IRINGA** | 1 | 2 | 1 | 2 | 1 | 1.4 |
| 86 | Ludewa DC | **IRINGA** | 1 | 1 | 1 | 2 | 2 | 1.4 |
| 87 | Kigoma DC | **KIGOMA** | 0 | 2 | 2 | 1 | 2 | 1.4 |
| 88 | Moshi MC | **KILIMANJARO** | 1 | 2 | 2 | 1 | 1 | 1.4 |
| 89 | Rombo DC | **KILIMANJARO** | 2 | 2 | 2 | 1 | 0 | 1.4 |
| 90 | Kilwa DC | **LINDI** | 1 | 2 | 2 | 2 | 0 | 1.4 |
| 91 | Ruangwa DC | **LINDI** | 1 | 2 | 1 | 2 | 1 | 1.4 |
| 92 | Simanjiro DC | **MANYARA** | 1 | 1 | 1 | 2 | 2 | 1.4 |
| 93 | Ileje DC | **MBEYA** | 1 | 1 | 1 | 2 | 2 | 1.4 |
| 94 | Mbarali DC | **MBEYA** | 1 | 1 | 2 | 2 | 1 | 1.4 |
| 95 | Mbeya DC | **MBEYA** | 1 | 1 | 2 | 2 | 1 | 1.4 |
| 96 | Morogoro DC | **MOROGORO** | 2 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1.4 |
| 97 | Mvomero DC | **MOROGORO** | 2 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1.4 |
| 98 | Mtwara Mikindani MC | **MTWARA** | 2 | 1 | 1 | 1 | 2 | 1.4 |
| 99 | Magu DC | **MWANZA** | 1 | 2 | 1 | 2 | 1 | 1.4 |
| 100 | Kahama DC | **SHINYANGA** | 1 | 1 | 2 | 2 | 1 | 1.4 |
| 101 | Singida MC | **SINGIDA** | 1 | 2 | 1 | 2 | 1 | 1.4 |
| 102 | Korogwe DC | **TANGA** | 2 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1.4 |

| NAFASI | HALMASHAURI | MKOA | 2005/6 | 2006/7 | 2007/8 | 2008/9 | 2009/10 | ALAMA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 103 | Meru DC | **ARUSHA** | **N/A** | **N/A** | 1 | 1 | 2 | 1.3 |
| 104 | Bahi DC | **DODOMA** | **N/A** | **N/A** | 1 | 1 | 2 | 1.3 |
| 105 | Chato DC | **KAGERA** | **N/A** | **N/A** | 2 | 1 | 1 | 1.3 |
| 106 | Rorya DC | **MARA** | **N/A** | **N/A** | 2 | 1 | 1 | 1.3 |
| 107 | Nanyumbu DC | **MTWARA** | **N/A** | **N/A** | 1 | 1 | 2 | 1.3 |
| 108 | Mkinga DC | **TANGA** | **N/A** | **N/A** | 2 | 1 | 1 | 1.3 |
| 109 | Arusha MC | **ARUSHA** | 1 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1.2 |
| 110 | Monduli DC | **ARUSHA** | 1 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1.2 |
| 111 | Ngorongoro DC | **ARUSHA** | 1 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1.2 |
| 112 | Mkuranga DC | **COAST** | 1 | 1 | 1 | 2 | 1 | 1.2 |
| 113 | Makete DC | **IRINGA** | 1 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1.2 |
| 114 | Njombe DC | **IRINGA** | 1 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1.2 |
| 115 | Kigoma/Ujiji MC | **KIGOMA** | 1 | 1 | 1 | 1 | 2 | 1.2 |
| 116 | Moshi DC | **KILIMANJARO** | 1 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1.2 |
| 117 | Liwale DC | **LINDI** | 1 | 1 | 1 | 2 | 1 | 1.2 |
| 118 | Babati DC | **MANYARA** | 1 | 1 | 1 | 2 | 1 | 1.2 |
| 119 | Mbeya CC | **MBEYA** | 0 | 2 | 2 | 1 | 1 | 1.2 |
| 120 | Kilosa DC | **MOROGORO** | 2 | 2 | 1 | 0 | 1 | 1.2 |
| 121 | Mwanza CC | **MWANZA** | 1 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1.2 |
| 122 | Ukerewe DC | **MWANZA** | 1 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1.2 |
| 123 | Sumbawanga MC | **RUKWA** | 0 | 2 | 2 | 1 | 1 | 1.2 |
| 124 | Namtumbo DC | **SONGEA** | 1 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1.2 |
| 125 | Kishapu DC | **SHINYANGA** | 1 | 1 | 2 | 2 | 0 | 1.2 |
| 126 | Korogwe TC | **TANGA** | 1 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1.2 |
| 127 | Lushoto DC | **TANGA** | 1 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1.2 |
| 128 | Nzega DC | **TABORA** | 1 | 1 | 1 | 2 | 1 | 1.2 |
| 129 | Sikonge DC | **TABORA** | 1 | 1 | 2 | 1 | 1 | 1.2 |
| 130 | Longido DC | **ARUSHA** | **N/A** | **N/A** | 1 | 1 | 1 | 1.0 |
| 131 | Chamwino DC | **DODOMA** | **N/A** | **N/A** | 1 | 1 | 1 | 1.0 |
| 132 | Mwanga DC | **KILIMANJARO** | 1 | 2 | 1 | 1 | 0 | 1.0 |
| 133 | Masasi TC+ | **MTWARA** | 1 | 1 | **N/A** | **N/A** | 1 | 1.0 |
| 134 | Igunga DC | **TABORA** | 0 | 2 | 1 | 1 | 1 | 1.0 |
| 135 | Kondoa TA | **DODOMA** | 3 | 2 | **N/A** | **N/A** | **N/A** | 2.5* |
| | **Alama ya Wastani wa Jumla** | | 1.4 | 1.8 | 1.5 | 1.6 | 1.4 | 1.5 |
| | **Jumla ya Halmashauri Zilizokaguliwa** | | **124** | **124** | **133** | **133** | **134** | |

## Mfumo wa rangi na maelezo ya alama

| | |
|---|---|
| 3 | Safi (Inayoridhisha) bila masuala ya msisitizo |
| 2 | Safi (Inayoridhisha) yenye masuala ya msisitizo |
| 1 | Si safi (Yenye shaka) |
| 0 | Mbaya |

N/A: Mamlaka ya Serikali ya Mtaa haikuwapo/haipo kwa jina hilo katika mwaka wa ukaguzi. Kwa halmashauri zilizokaguliwa kwa chini ya miaka mitano, alama ya wastani kwa miaka mitatu inadhaniwa kuwa ndiyo nzuri zaidi ambayo wangeweza kupata kama ukaguzi ungefanyika kwa miaka mitano.

*Mamlaka ya mji wa Kondoa haikujumuishwa katika kukokotoa alama ya jumla.

+ Kabla ya mwaka 2009/10 ilikuwa mamlaka ya mji

**Chanzo cha data:** Ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuhusu hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa